



TANGAZO LA ZABUNI

MWALIKO WA ZABUNI YA URASIMISHAJI WA MAKAZI KATA YA MAJENGO KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJJIJI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

TAREHE: 30/08/2019

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji kwa niaba ya Kamati ya urasimishaji makazi Kata ya Majengo anapenda kuwatangazia wananchi wote kazi ya kurasimisha makazi 4329 yaliyoko katika Manispaa ya Kigoma Ujiji. Lengo ni kuawezesha wananchi kupata viwanja vilivyopimwa, kusajiliwa na kupata hati miliki za ardhi. Mradi huo utagharamiwa kwa michango ya wakazi wanaorasimishiwa makazi yao kupitia kamati ya urasimishaji ya wananchi.

NAMBA YA ZABUNI	AINA YA ZABUNI	GHARAMA YA MAOMBI KWA KILA ZABUNI
LGA/042/2019/2020/NC/17	Urasimishaji wa makazi kata ya Majengo	TZS 100,000.00

Mwombaji anatakiwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:-

1. Kivuli cha Leseni ya Biashara halali na iliyo hai.
2. Kampuni iambatanishe kivuli cha Cheti cha usajili (Certificate of Registration)
3. Awe na cheti cha usajili wa Kampuni kutoka Bodi ya upangaji na upimaji (TPRB, NATLS)
4. Kivuli cha Utambulisho wa mlipa kodi (TIN namba au VAT).
5. Aweke stakabadhi halisi ya malipo ya maombi.
6. Hati halisi ya uthibitisho wa uwakilishi wa ki-sheria (Power of attorney)
7. Kivuli cha Taarifa za kibenki (Bank statements) za miezi mitatu inayoishia July 2019.
8. Kivuli cha Taarifa za Kampuni (Company Profile) .
9. Awe na wataalamu wenye sifa zinazostahili

MASHARTI KWA MWOMBAJI:

1. Zabuni itafanyika kwa njia ya ushindanishi (National Competitive Bidding) Kama ilivyoelezwa kwenye kanuni za manunuzi (Goods, Works, Non Consultant Services and disposal of Public Assets by Tender), 2013- Tamko la Serikali Na. 446
2. Kila mwombaji atalipa ada ya maombi ya zabuni ambayo haitarudishwa na kila ombi ni zabuni inayojitegemea na italipiwa kiasi cha ada kilichoainishwa katika akaunti na. **51610000197 NMB kwa jina la Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.**
3. Mwombaji anaweza kupata maelezo zaidi katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni , Manispaa ya Kigoma Ujiji, S.l.p 44 iliyoko eneo la Mnarani kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa siku za kazi.
4. Watakaopata zabuni watatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.
5. Zabuni zote ziambatane na tamko la dhamana ya zabuni ambalo litakuwepo kwenye kabrasha la zabuni
6. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha zikiwa ni **"ORIGINAL MOJA NA COPY MBILI"** (kwa Lakiri). Juu ya bahasha ioneshe aina ya zabuni, namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji,**

S.L.P. 44, KIGOMA

7. Vigezo vya tathmini ya zabuni zote ni kama ilivyoainishwa kwenye tangazo pamoja na kwenye kabrasha za kila zabuni.
8. Bodi ya zabuni haitalazimika kukubali zabuni ambayo gharama zake ziko juu au chini sana. (Vigezo vya Sheria ya manunuzi ya 2011, Kanuni zake za 2013 pamoja na marekebisho yake vitazingatiwa).
9. Zabuni zitakazochelewa kuwasilishwa katika muda uliopangwa hazitapokelewa.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya zabuni hizo ni **Alhamis ya tarehe 16 September 2019** ambayo ndiyo itakuwa siku ya ufunguzi wa zabuni hizo saa **5.00 asubuhi**, katika ukumbi wa **Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji**. Mwombaji au mwakilishi wake wanakaribishwa katika ufunguzi wa zabuni hizo.


Mwalika S. Pangani

**Mkurugenzi wa Manispaa
KIGOMA UJJI**

**MKURUGENZI WA MANISPAA
KIGOMA/UJJI**

**MKURUGENZI WA MANISPAA
KIGOMA/UJJI**